**SHDEPHA+ NETWORK FOR PLHA, KAHAMA BRANCH, P.O BOX 564, KAHAMA, TEL: 028-2710730, MOB: +255 785 820 330** Email: shdephakahama@yahoo.com

# TANGAZO LA TENDA YA KUSHONA SARE ZA SHULE KWA WANAFUNZI WA SHULE ZA MSINGI.

**UTANGULIZI**

SHDEPHA+ Ni Shirika lisilo la kiserikali, Limesajiliwa Tarehe 21/11/1994 kwa Nambari ya Usajili 8216. Shdepha + Ina matawi zaidi ya 5 kote nchini.shirika la SHDEPHA + Limekuwa Likifanya Kazi na Wahisani Wote wa Kitaifa na kimataifa , Serikali kuu na serikali za Mitaa, na Wadau mbali mbali katika utekelezaji wa Shughuli zake za kuihudumia jamii kupitia miradi mbali mbali ya kiafya ikiwemo UKIMWI,KIFUA KIKUU,MALARIA, ELIMU na miradi inayohusiana na maswala mazima ya UJINSIA .

SHDEPHA + kwa kushirikiana na Pact-Tanzania inatekeleza Mradi wa USAID ACHIEVE katika Halmashauri za Msalala, Kahama mji na Ushetu.Kupitia Mradi huu, SHDEPHA + imepanga kutoa ufadhili wa Sare za Shule kwa wanafunzi 411 wa shule za Msingi kutoka kaya zenye mazingira magumu. Lengo la ufadhili huu nikuongeza Morali ya wanafunzi lengwa kuhudhuria shule, kujifunza kikamilifu nakupunguza utoro unaosababishwa na kukosa sare. Ni imani yetu kuwa endapo wanafunzi hawa watapatiwa sare siyo TU morali ya kuhudhuria shule itaongezeka ila pia ufanisi wao katika masomo utaongezeka maradufu. Kwa Mantiki hiyo, SHDEPHA + inapenda kuwatangazia watu wote wenye sifa na uwezo; binafsi, Vikundi au Makampuni wanaojishughulisha na kazi za kushona na kusambaza sare za Shule ndani ya wilaya ya Masasi kutuma Maombi ya tenda ili kutimiza lengo hilo la kuwapatia wanafunzi Sare.

**SIFA ZA MWOMBAJI**

1. Awe anaendesha shughuli zake katika Wilaya ya Msalala, Ushetu na Kahama mji. Uthibitisho wa hili ni ***Barua ya utambulisho kutoka Mtendaji wa Kata/Mtaa/kijiji anakofanyia kazi***

2. Awe na Uzoefu wa kutosha kukamilisha kazi kwa ubora unaokubalika (**Uthibitisho wa kazi sawa na hii kwa siku za nyuma- ambatanisha wasifuwako**).
3. Awe na Uwezo wa kukamilisha kazi ya kushona Sare zote kwa muda mfupi usiozidi wiki mbili (***uthibitisho wa uwepo wa vifaa na Rasirimali watu wa kutosha kuonyesha idadi ya vyerehani na wafanyakazi ulionao pia ambatanisha mpango kazi wako***).
4. Awe anaijua vizuri jiografia ya Halmashauri ya Wilaya ya Kahama, Msalala na Ushetu (ufahamu wa shule na aina ya Sare zinazotumiwa)

**MASHARTI MAHUSUSI**

1. Uwezo wa kutoa huduma hadi kukamilika bila kuhitaji Malipo ya awali (Malipo yatafayika baada ya kazi kukamilika)
2. Uwezo wa kushona Sare kwa kuuzingatia ubora na vigezo vilivyokubaliwa (kutumia kitambaa, Vishikizo, zipu na nyuzi zenye ubora wa juu)
3. Mhusika ni lazima awe na Risiti ya EFD (risiti ya Mashine) au barua ya Msamaha wa kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania au Kitambulisho cha Mjasiriamali
4. Awe na uwezo wa kuwasilisha sampuli ya kitambaa kitakachotumika, bei halisi ya kushona na kusambaza Sare kwa walengwa kwa muda uliokubaliwa.
5. Kuzingatia bei halisi ya soko ya kushona, kununua na kusambaza Sare husika kwa walengwa (wanafunzi wa shule za Msingi zilizopo ndani ya H/mashauri ya wilaya ya Msalala, Kahama na Ushetu)
6. Uwezo wa kukamilisha zoezi la kushona na kukabidhi sare husika kwa walengwa ndani ya siku 14 tangu kusainiwa mkataba. Jumla ya wanafunzi ni 411 ambapo wanafunzi 411 (ME 207, KE 204) ni wa shule za Msingi.

**MAANA YA SARE KWA MUJIBU WA TANGAZO HILI**

Kwa Mujibu wa Tangazo hili Sare za Shule itamaanisha

a) Shati moja, kaptura moja kwa wavulana

b) Shati moja na Sketi Moja kwa wasichana

c) Soksi Pea mbili kwa wavulana na wasichana

d) Sweta moja kwa wavulana na wasichana.

e) Viatu vyeusi pea moja kwa wasichana na wavulana.

**NAMNA YA KUTUMA MAOMBI**

Maombi yatumwe yakiwa kwenye bahasha iliyofungwa vizuri kwenda kwa Mkurugenzi SHDEPHA + KAHAMA S L P 564 Kahama. Kwa njia ya mkononi inakubalika pia.

**MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI**

Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha maombi ni **05/6/2022** Saa kumi na moja jioni

SHDEPHA+ INAFANYA KAZI KWA KUZINGATIA MISINGI MBALIMBALI IKIWEMO HAKI ZA WATOTO,KUPINGA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU NA KUWAKUZINGATIA MAADILI YA SHIRIKA ,HIVYO WAZABUNI WOTE WATAKOVUTIWA NA ZABUNI HII WATATAKIWA KUFUATA MISINGI YASHIRIKA KAMA ILIVYOAINISHWA HAPO CHINI.

- Kukubali kufanyiwa ukaguzi wa kutokuwekewa masharti yakufanya kazi na USAID ( Supplier vetting)
- Kutojihusisha kwa namna yoyote na biashara haramu ya usafirishaji binadamu( Anti trafficking)
- Kutojihusisha na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa namna yoyote –hii hujumuisha wafanyakazi wote kwa mzabuni atakayechaguliwa.
- Kutojihusisha naukiukaji sheria zinazomlinda mtoto(chini ya miaka 18)

Kwakuzingatia hili mzabuni/wazabuni watakao chaguliwa watatakiwa kudhibitisha uelewa nakutojihusisha na mambo hayo yaliyoainishwa hapo juu.

Tarehe za mchakoto huu wa zabuni

| Maelezo | Tarehe |
|---|---|
| Mwaliko wa zabuni | 23/5/2022 |
| Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha maombi | 05/6/2022 |
| Ufunguzi wa zabuni | 07/6/2022 |
| Kamati ya mapitio ya zabuni | 08/6/2022 |
| Ukaguzi, tathmin na majadiliano | 08/6/2022 |
| Kutoa zabuni | 10/06/2022 |